# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mupango ya usalama

**Mwongozo ya kusaidia jamaa kujitayarisha kwa kukabiliana na hali ya kukamatwa ao kufungiwa na maafisa wa uhamiaji.**

## MAELEKEZO YA USALAMA

- Weka namba yako ya uhamiaji (A-Namba) mu kichwa.
- Epuka kutembelea jela na magereza.
  - Maafisa wa uhamiaji wanaweza kushirikiana na polisi wa eneo ao wa jimbo kwa kutafuta batu benye habako banainchi ba Marekani mu jela na mu magereza.
- Epuka fasi za batu bote zenye zinajulikana kuwa za hatari ao zenye zinajulikana kama fasi kwenye batu benye habako banainchi ba Marekani banazoweyaka kusanyika.
  - Ni rahisi zaidi kwa polisi kukukamata kama uko ku fasi ya batu bote tofauti na kama ungelikuwa kunyumba.
- Elezea batu benye unaishi nabo munyumba kuhusu haki zao.
  - Hakikisha jamaa yako, watoto wako, na batu bengine benye banaishi mu nyumba yako banajua haki zao. Bashirikishe mu habari yenye inapatikana mu mwongozo ya "**Jua Haki Zako**".



## MAHITAJI YA AFYA

- Kama uko na shida ya afya, andikisha kadi yako na uibebe kila wakati yenye inaonyesha hali yako ya afya pamoya na majina na dozi za dawa zenye unatumia.
- Muelezeye mutu mwenye unaamini kuhusu hali yako ya afya na msaada yenye unahitaji.
- Kumbuka kusaini fomu ya HIPAA kusudi umupatiye ule mutu ruhusa ya kuona habari zako za afya, kukukamatiya dawa na kuzungumuza na munganga wako kuhusu mahitaji yako ya afya.

## MUPANGO WA PESA

- Mujulishe mwanainchi wa Marekani ao mutu muzima mukaaji mwenye anaruhusiwa kisheria kuishi Marekani kwa muda murefu mwenye unaamini habari za akaunti yako ya benki ao kwenye unawekeaka pesa yako. Hii itakusaidiya kuhakikisha kama pesa yako inachungiwa muzuri hata wakati unafungiwa ao ukifukuzwa mu inchi. Bila mupango, unaweza kushindwa kulipa bili, malipo ya nyumba na malipo ya masomo. Watoto na jamaa yako watahitaji pesa za kuendelea kuishi mu nyumba na kuuza chakula.
- Unaweza kumupatiya mutu mwenye unaamini mamulaka ya kisheria ya kukuwakilisha kusudi akusaidie kufanya maamuzi kuhusu pesa yako. Hii itamuruhusu kulipa bili, kuweka pesa mu benki na kulipa kwa ajili ya kuachiliwa yako kwa muda kama itahitajika.
- Hakikisha watoto na jamaa yako wako na pesa ya kutumikisha mu hali ya zarura.

# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mupango ya usalama

**Mwongozo ya kusaidia jamaa kujitayarisha kwa kukabiliana na hali ya kukamatwa ao kufungiwa na maafisa wa uhamiaji.**



## HUDUMA ZA MALEZI YA WATOTO

- Chagula mwanainchi wa Marekani ao mutu muzima mukaaji mwenye anaruhusiwa kisheria kuishi Marekani kwa muda murefu mwenye unaamini mwenye atakuwa tayari kukuwa mlezi wa watoto wako kama unafungiwa ao ukifukuzwa mu inchi. Hakikisha hii uamuzi imeandikwa mu hati zenye zinafaa. Kila jimbo iko na sheria zake kuhusu malezi ya watoto na mamulaka ya kisheria, hii inaweza lomba mutu abebe zile hati ku ofisi ya jimbo ao mahakama ya jamaa.
- Mupatiye mutu mwenye unaamini habari kuhusu masomo ya watoto wako, hali zao za afya na namba zingine za zarura.
- Waelezeye watoto wako kuhusu mupango. Hakikisha wako na namba za zarura na wanajua ni nani wanaweza kuwasiliana naye.

## WEKA HATI ZAKO SALAMA

- Weka fasisalama nakala za asili za hati zako za uhamiaji, zikiwa amo visa, barua za ombi, risiti, ilani, pasipoti na vibali ya kazi.
- Weka pia nakala mu simu yako.
- Kama uko na kesi ya uhamiaji yenye inaendelea, sawa vile ombi la hifazi, endelea kukusanya na kusasisha ushuhuda yako.
- Weka nakala za asili za tiketi za trafiki, risiti za malipo na hati za mahakama pamoya na rekodi za makosa ya uhalifu, kama ziko. Kama hauna azo, zilombe kutoka kwenye kaunti, jimbo ao mahakama yenye inahusika.
- Hakikisha jamaa yako, mwanasheria wako na batu bengine benye unaamini banajua fasi kwenye zile hati zinawekewa.



## MSAADA WA KISHERIA

- Weka mu kichwa ao weka  namba ya simu na barua pepe ya mwanasheria wak
- Kama hauna mwanasheria, weka mu kichwa ao weka namba ya simu ya ofisi ya wanasheria ao shirika yenye inatoa msaada wa kisheria bila malipo.
- Waelezeye watoto wako, jamaa yako na batu benye unaamini kuhusu hizi habari.
- Ukuwa na oroza ya namba za simu na anuani za vituo ya kufungiya amo wahamiaji, kituo cha polisi, jela na gereza ya karibu. Elezeya jamaa yako na batu benye unaamini kuhusu hii oroza.